# TNMC Habari

Toleo No. 0021

TOLEO MAALUMU Agosti.2025

HALIUZWI www.tnmc.go.tz @tnmchabari


# Mahafali Ya (14) Ya Wauguzi Na Wakunga Kufanyika Septemba 17.2025 Jijini Dodoma UK. 01






## Timu ya Uongozi TNMC Yapigwa Msasa Uandaaji wa Hesabu Katika Sekta za Umma

UK. 08



## TNMC: Wenye nia Ya Kusoma Taaluma za Uuguzi na Ukunga Zingatieni Sifa za Kujiunga

UK. 03



## Wauguzi, Wakunga Wajadili Uhuishaji Leseni za Kitaaluma ya Mwaka wa Fedha 2025/2026

UK. 7

# Mahafali ya (14) ya Wauguzi na Wakunga Kufanyika Septemba 17.2025 Jijini Dodoma

*Na Mwandishi Wetu*





**Zaidi ya wauguzi na wakunga 2080 Waliofaulu Mtihani wa usajili na Leseni uliofanyika tarehe 23 Mei 2025 Wanatarajiwa kutunukiwa vyeti vya usajili na Leseni na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TNMC tarehe 17 Septemba 2025, katika hafla ya mahafali ya 14 inayotarajiwa kufanyika Jijini Dodoma katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Chimwaga) uliopo Chuoni hapo.**

**Taarifa ya Msajili wa Baraza iliyotolewa na kitengo cha habari na Mawasiliano kwa umma, imeeleza kuwa katika Mahafali hayo, mada mbalimbali zenye lengo la kuwakumbusha, maadili, miiko, Sheria na kanuni za utendaji kazi katika taaluma hiyo, zitatolewa kabla ya wataaluma hao kula kiapo cha uadilifu na utoaji huduma unaozingatia weledi na upendo.**

**Aidha, taarifa hiyo imemtaka kila Mwanataaluma kuzingatia taratibu kwa kuvaa Sare ya Kitaaluma *"Professional Uniform"* iliyoidhinishwa na TNMC ikiwa ni pamoja na: -**

1. **WANAWAKE- Kuvaa Magauni au Suruali na Blauzi rangi nyeupe ndefu.**
2. **WANAUME- Kaunda suti- Shati jeupe na suruali dark blue**
3. **VIATU- Vinavyofunika miguu na siyo vya wazi, viwe vya rangi nyeusi, nyeupe au brown.**
4. **Kitambulisho cha Indexing au NIDA au Kitamburisho cha Mpiga kura chenye picha ya mhusika/ kinachomtambulisha, Sandozi au Kandambili haviruhusiwi**

**Mahafali hiyo inatarajiwa kuanza asubuhi ya saa 01:00 ikiwa ni Mahafali ya 14 tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa halfa hiyo muhimu ya kitaaluma.**

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TMNC ni mamlaka ya kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za uuguzi na ukunga Tanzania, Chini ya Sheria ya Uuguzi na ukunga ya mwaka 2010 na kanuni zake *(The Nursing and Midwifery Act 2010)* ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini zinakiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.**

# TANGAZO

## CPD ZINAZOKUBALIKA KATIKA UHUISHAJI LESENI ZA KITAALUMA

Ukiwa na CPD Point 60 za eneo moja la Mafunzo ambayo yanayopatikana Eneo la kazi (NON ACCREDITEED CPD) zinatosha kuhuisha Leseni yako. ✔

Ukiwa na CPD Point 60 za eneo moja la Mafunzo yaliyoratibiwa na kupata Ithibati (ACCREDITEED CPD) zinatosha kuhuisha Leseni yako ✔

Ukiwa na CPD Point 60 za eneo moja la Mafunzo yanayopatikana kwa njia ya Mtandao (ONLINE CPD) HAZITOSHI kuhuisha Leseni. X

HAPA ni point 12 tu! ambapo mtaaluma anatakiwa kupata alama 4 kwa mwaka

**HATA UKICHANGANYA NON ACCREDITED + ACCREDITED + 12 POINT ZA ONLINE = 60 POINT ( ZINAKUBALIWA)**

***#LESENI YANGU AJIRA YANGU***

# TNMC: Wenye nia Ya Kusoma Taaluma za Uuguzi na Ukunga Zingatieni Sifa za Kujiunga



Na Mwandishi Wetu

Imeelezwa kuwa Mtu yeyote anayependa kusomea taaluma za uuguzi na ukunga nchini na nje ya nchi kufahamu sifa zinazohitajika na inapobidi kupata ushauri kutoka ofisi ya Msajili wa Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania TNMC, ili kuepuka vikwazo vya kutokusajiliwa na Baraza mara baada ya kuhitimu masomo katika vyuo vya ndani na nje ya nchi.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Mafunzo na maendeleo ya taaluma wa Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania Bi. Happy Masenga, alipokuwa akizungumza na TNMC habari Ofisini kwake Jijini Dodoma baada ya Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanataaluma ambao huomba kusajiliwa na Baraza wakati hawana sifa za kusajiliwa ili kutoa huduma kwa jamii.

***"Napenda kutumia fursa hii kuwajulisha wanataaluma wote wanaojiunga na mafunzo katika vyuo vyote vya ndani na nje ya nchi, kuhakikisha wanazingatia sifa za kujiunga na vyuo kwa mujibu wa vigezo vilivyopo kwenye mitaala ili kupata umahiri katika maeneo ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga kwa ngazi husika."***

***"Ofisi inashauri kuwasiliana na Baraza ili kupata ufafanuzi na ushauri juu ya aina ya kozi sahihi unayotakiwa kusoma kama muuguzi au Mkunga ili kuepuka usumbufu unaweza kujitokeza wakati wa usajili na Leseni, Baraza haliwezi kumsajili na kumpatia leseni mtu ambaye hana sifa kwa kuwa usajili ni kwa mujimu wa Sheria ya uuguzi na ukunga sanjari na kanuni zake"***

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania lilianzishwa chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga Na.1 ya mwaka 2010 na Kanuni zake pamoja na Miongozo mingine, Baraza limepewa mamlaka ya kuhifadhi na kulinda usalama wa afya ya jamii kwa kuhakikisha kuwa inasimamia mafunzo ya Uuguzi na Ukunga pamoja utoaji huduma kutoka kwa wataalamu waliyokidhi vigezo.

Aidha, jukumu lingine la Baraza ni:- Usajili wa wataaluma ni kwa mujibu wa kifungu Na.15(1) b cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga.



# MAKALA MAALUMU

## Fahamu Sababu za Kujifungua kwa njia ya Upasuaji (Caesarean Section) Dhidi ya njia ya kawaida (Normal Vaginal Delivery)




**MAKALA HII IMEANDALIWA NA TNMC HABARI, CHINI YA MKUNGA MBOBEZI BI. MWAJUMA MUTABAZI WA TNMC**

### Sababu za Mama mwenyewe:

- Mama mjamzito mwenye shinikizo kubwa la damu linaweza kupelekea ulazima wa Mama huyu kuondolewa Mtoto wake kabla ya wakati ili kuepusha athari zinazoweza kusababisha madhara ya kudumu kwake na Mtoto wake.

- Kisukari ikijumuisha Gestational Diabetes Mellitus
Mama anayebeba ujauzito akiwa na ugonjwa wa Kisukari au anayepata gonjwa huo wakati tayari ana ujauzito (GDM) unapelekea Mtoto kuwa mkubwa sana ***(Fetal macrosomia)***

- Matatizo ya moyo na ujauzito: hupelekea Mama kuhitaji kutunzwa chini ya uangalizi maalum na hufanyiwa upasuaji ili kuepuka hatari zinazoweza kutokea ikiwa atakaa kwenye uchungu kwa muda mrefu

- Kuyumba kwa mapigo ya Moyo ya Mtoto ***(NonReassurance Fetal Heart Rate)*** au matatizo ya ukuaji tumboni hulazimika kuzalishwa kwa upasuaji

- Umbile la nyonga ya Mama kutofautiana na kitangulizi cha Mtoto ***(Cephalopelvic Disproportion – CPD)***, au Mama kuwa na ulemavu wa nyonga, uvimbe kwenye nyonga au ugonjwa ulioathiri njia ya kawaida ya uzazi ***(Extensive Vaginal Wats).***

- Mama aliyewahi kujifungua kwa upasuaji: Hasa zaidi ya mara moja, ni kiashiria kikubwa cha kuendelea kukifungua kwa njia hiyo kutokana na hatari ya kupasuka kwa nyumba ya kizazi ***(Uterine rupture)***

- Uchungu usioridhisha pamoja na uchungu pingamizi: Mama anaweza kuanza uchungu lakini mlango wa kizazi usifunguke ipasavyo au Mtoto asishuke, hii hupelekea Mama kuhitaji upasuaji.

### Sababu za Mtoto:

**Mtoto kulala vibaya tumboni**
***(Malpresentation and Malposition)***
Mtoto aliyelala upande baada ya wiki ya 37 ya ujauzito ***(transverse lie)*** kutanguliza makalio hasa katika ujauzito wa kwanza ***(breech presentation)*** au kuingia kwenye nyonga na diameter kubwa ni sababu ya mama kuhitaji upasuaji ili kuhakikisha usalama wa wote.

Mapigo ya moyo ya mtoto kubadilika katikati ya uchungu ***(Fetal Distress/ NonReassurance Fetal Heart Rate)*** huhitaji upasuaji wa dharura.

Mimba ya watoto mapacha waliothibitika kuwa wakubwa au kulala vibaya, mimba yenye matatizo ya kondo la nyuma kutangulia au kujiengua mapema ***(Placenta Previa and Placental Abruption)*** huhitaji upasuaji wa dharura.

| Njia ya Kawaida | Njia ya upasuaji |
|---|---|
| Njia hii ni salama zaidi ikiwa hakuna matatizo ya kiafya kwa mama na mtoto wake kwa sababu huchukua muda mfupi kupona na madhara yake madogo. | Usalama wa njia hii huwa ni pale kunapokuwa na matatizo yanayohatarisha maisha ya mama au mtoto ila ikumbukwe kuwa ni upasuaji mkubwa wenye hatari za maambukizi, kumwaga damu nyingi pamoja na madhara ya dawa za usingizi |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**




@tnmchabari www.tnmc.go.tz 0736 00 60 60

# Watanzania Kunufaika na Tiba Asili Zilizochanganyika na Sayansi na Urithi wa Asili

*Na Mwandishi Wetu*



Watanzania wanatarajia kunufaika zaidi na huduma za tiba asili na tiba mbadala baada ya Serikali kuimarisha mfumo wa usimamizi, utafiti na upatikanaji wa dawa salama na zenye viwango vya kitaalamu.

Hayo yamebanishwa Agosti 29, 2025 na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Khatibu Kazungu katika maadhimisho ya Siku ya Tiba Asili ya Mwafrika yaliyofanyika Dodoma, alipokuwa akimwakilisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa.

Dkt. Kazungu amesema wananchi sasa wanapata huduma jumuishi za tiba asili katika hospitali 14 za mikoa, hali inayowawezesha kuchagua kati ya tiba za kisasa, tiba asili au kutumia zote kwa pamoja.

"Huduma hii inamuwezesha mteja kufanyiwa vipimo vya kitaalamu na kupewa ushauri sahihi kuhusu tiba itakayomfaa. Hii inaleta faraja kubwa kwa wananchi kwani sasa tiba asili inapatikana kwa usalama zaidi ndani ya mfumo wa hospitali zetu," amesema Dkt. Kazungu.



Dkt. Kazungu amesema Wananchi pia watanufaika na ajira mpya kutokana na kuanzishwa kwa kiwanda cha kuzalisha dawa za tiba asili cha NIMR-Mabibo, ambacho kitategemea malighafi kutoka kwa wakulima wa miti dawa.

Aidha, amesema Serikali imeboresha usindikaji na ufungashaji wa dawa za tiba asili, na sasa zaidi ya dawa 141 zimesajiliwa huku zingine 42 zikiwa zimefanyiwa tafiti za usalama na ubora.

Kwa wananchi wanaotumia tiba asili, Dkt. Kazungu amesema hatua hizi zinamaanisha kupata huduma zilizo salama zaidi, zenye ubora unaokubalika na bei nafuu.

Amesema kwa mujibu wa Rais Samia Suluhu Hassan, maendeleo haya ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050 inayolenga kuhakikisha Watanzania wanapata afya bora kupitia urithi wa tiba za asili na sayansi ya kisasa.

# Wauguzi, Wakunga Wajadili Kidigitali namna ya Uhuishaji Leseni za Kitaaluma Mwaka wa Fedha 2025/2026



*Na Mwandishi Wetu*

Kurugenzi ya Usajili, Maadili na Leseni ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania katika kipindi cha mwezi Agosti, 2025 imeendelea kuongoza vikao kazi kwa njia ya mtandao juu ya Uhuishaji leseni na CPD vikao ambavyo vimewajumuisha viongozi kada hizi mbili pamoja na wauguzi na wakunga kwa ujumla. .

Uratibu wa vikao umeendelea kufanyika kwa njia ya mtandao kutoka mkoa mmoja baada ya mwingine, lengo ikiwa kukumbushana taratibu za zoezi la uhuishaji leseni za kitaaluma na mafunzo ya CPD hususani katika mwaka huu wa Fedha ambapo kunakundi kubwa la wauguzi na wakunga takribani elfu 30 wanaotakiwa kuhuisha leseni zao kwa mujibu wa Sheria ya uuguzi na ukunga ya mwaka 2010.

Aidha, zoezi hili huenda sambamba na mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma (CPD) ambapo Mafunzo haya pia ni takwa la kisheria katika Sheria ya uuguzi na ukunga ya mwaka 20210 na kanuni zake kifungu cha 06 (28)(01) ambapo wataaluma hutakiwa kufanya maendeleo endelevu ya umahiri wao wa kitaaluma kwa kumtaka muuguzi na mkunga kujiendeleza kitaaluma ikiwa ni kigezo muhimu wakati wa kuhuisha Leseni yake bila kujali kama ameajiriwa, amejiajiri au hajaajiriwa na hili inaenda sambamba na sera ya Kitaifa inayohimiza mafunzo ya Kitaalamu kwa Watoa Huduma za Afya Tanzania ya mwaka 2016 ***(National CPD Framework, 2016).***

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania, chini ya Sheria ya Mwaka 2010 (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.



# Timu ya Uongozi TNMC Yapigwa Msasa Uandaaji wa Hesabu Katika Sekta za Umma



*Na Mwandishi Wetu*

**Menejimenti ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania imepata mafunzo kuhusu uandaaji wa ripoti endelevu na mafunzo ya viwango vya kimataifa jinsi ya uandaaji wa hesabu za sekta ya umma (IPSAS) mafunzo ambayo yamefanyika Jijini Dodoma katika Ofisi za TNMC.**

**Mafunzo hayo yaliyotolewa na Mkufunzi kutoka taasisi ya Ernest and Young CPA Dr. Neema Kiure, mwanzoni mwa mwezi Agosti.2025 ambapo alianza kwa kufafanua maana ya IPSAS akibainisha kuwa ni kifupi cha (*International Public Sector Accounting Standards)* Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma ambapo viwango vya kimataifa vinavyotolewa na IPSASB *(International Public Sector Accounting Standards Board)* chini ya IFAC *(International Federation of Accountants).***

**Aidha, CPA Neema, aliongeza kuwa,lengo lake ni kuziongoza taasisi za umma,serikali kuu, serikali za mitaa, mashirika ya umma katika kuandaa taarifa za kifedha zilizo wazi, sahihi na zinazolingana kimataifa na husaidia**



**kuongeza uwazi *(transparency)*, uwajibikaji *(accountability)*, na ulinganishaji *(comparability)* wa taarifa za kifedha za sekta ya umma.**

**Hata hivyo, umuhimu wa mafunzo hayo ni kurahisisha ulinganishaji wa taarifa za kifedha za nchi mbalimbali, inaimarisha usimamizi wa rasilimali za umma na huwezesha wadau Bunge, Wananchi, wahisani, n.k. kupata taarifa za kweli na sahihi kuhusu fedha za umma.**

# TANZIA

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi AGOSTI, 2025, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.**



**JINA: MARIAMU MKANYAMA**
**KITUO: MTWARA RRH**
**MKOA: MTWARA**



**JINA: DAINA MGENI**
**KITUO: ZAHANATI YA ZENGERENDETE**
**MKOA:NJOMBE**

*"Daima **Tutawakumbuka** Wapendwa **Wetu**"*

**WAWEZA KUWASILIANA NASI KWA**

**WhatsApp**

**0737 96 26 91**

# "Kutoka Dawati la Mhariri Mkuu



Karibu ujisomee Jarida la Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), lililo katika mfumo wa nakala laini, linaloandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Jarida hili linatolewa kila Mwezi likiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano wenye lengo la kuhabarisha Umma jinsi Baraza linavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

Habari na matukio tuliyokuandalia katika Jarida hili ni yale yanayohusu taaluma ya Uuguzi na Ukunga na Afya kwa ujumla.

Ikumbukwe kuwa, Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania, chini ya Sheria ya Mwaka 2010 ***(The Nursing and Midwifery Act, 2010)*** ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

**Ninakutakia usomaji mwema.**
**Asante sana**

**Bi.Agnes Mtawa**
**Msajili Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania**

## TIMU YA WAHARIRI WA JARIDA

| | |
|---|---|
| Bi. Agnes Mtawa | MWENYEKITI |
| Mwakapiso Ndimmyake | MHARIRI |
| Ezekiel Nyalusi | MSANIFU JARIDA |
| Irene Chilewa | MRATIBU |
| Rose Mhando | MRATIBU |

Tufuatilie katika

# Mitandao yetu ya Kijamii

@tnmchabari

LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA
www.tnmc.go.tz